## Sera ya Visu katika Shule

Wapendwa Wazazi na Walezi

Serikali ya NSW ilifanya mashauriano ya kijamii hivi karibuni, kushughulikia karibu na viongozi wa jamii ya Sikh na wataalum wa afya na usalama ili kurekebisha Sera ya Visu katika Shule.

Idara hiyo inashukuru watu wote wa jamii ambao walisema maoni yao wakati ya mashauriano na wale ambao walisaidia katika matengenezo ya miongozo iliyorekebishwa ambayo inaeleza hali ambayo mwanafunzi anaweza kuwa na kisu shuleni.

Miongozo hiyo inaonyesha ahadi ya idara kufanya inavyoweza ili kulinda wanafunzi na wafanyakazi dhidi ya hatari zinazoweza kutarajiwa kwa afya na usalama wao na ahadi yake kuheshima utofauti wa jamii ya NSW na kuepuka vitendo vya ubaguzi wa kinyume cha sheria.

Marufuku ya visu shuleni bado yanaendelea lakini hayazuii mwanafunzi kuvaa Kirpan mradi anafuata miongozo mikali mipya. Kirpan ni kitu, kinachofanana na kisu, ambacho kinavaliwa na watu wa Siku waliobatizwa kama kitu cha imani yao na ni cha muhimu sana ya kidini.

Kwa mwanafunzi wa Sikh aliyebatizwa kuruhusiwa kuvaa Kirpan shuleni, Kirpan kinapaswa:

- kuwa kidogo, urefu mzima wa 16.5cm (karibu 6.5 inchi) au chini, bila kingo au pointi kali
- kuwa na kengee ambayo imefungwa ndani ya ala ili isiweze kuondolewa
- kuvaliwa chini ya nguo na kuhifadhiwa ili hakiwezi kutumika
- kuondolewa na kuhifadhiliwa salama, au “kufungwa kwenye mwilini”, wakati anapofanya shughuli za kimwili kama vile michezo.

**Kumbuka:** “kufungwa kwenye mwilini” kuna maana ya kufungwa katika kitambaa chenye nguvu na kufungwa ndani ya bendi ya michezo au ukanda wa ngozi unaohakikisha hakiwezi kutoka au kusababisha kuumia kwa mvaaji au mtu mwingine.

Anapoulizwa kwa busara, mwanafunzi lazima athibitishe kwamba miongozo hii inafuatiliwa. Wasiwasi wowote wa usalama utajadiliwa na mwanafunzi na wazazi au watunzaji wake.

Wakati wanafunzi wa Sikh waliobatizwa wanaweza kuvaa Kirpan hawaruhusiwi kukitumia shuleni kwa madhumuni yoyote.

Wanafunzi hawaruhusiwi kuwa na kisu shuleni katika hali nyingine yoyote isipokuwa kisu kinatumiwa kwa madhumuni ya kielimu (kwa mfano wakati wa masomo ya vitendo ya teknolojia ya chakula).

Wanafunzi wanaoruhusiwa kuleta kisu shuleni kwa sababu wanahudhuria somo la TAFE mara moja baada ya shule wanahitaji kukabidhi kisu katika sanduku au ala kwa ofisi ya shule mwanzoni wa siku na kukikusanya mwisho wa siku.

Habari zaidi juu ya miongozi mipya inapatikana kwa https://education.nsw.gov.au/about-us/rights-and-accountability/legal-issues-bulletins/knives-in-schools

Ili kuwezesha kuanzishwa kwa sera mpya, ningeweza kufurahi kujadili mipango hii pamoja na viongozi na watu wa jamii yetu ya Sikh ya mtaani.

Familia za wanafunzi wa Sikh waliobatizwa wanaweza pia kutafuta mwongozo zaidi kupita hekalu lao kwa kushirikiana na Chama cha Sikh cha Australia (Australian Sikh Association (ASA)).

Ikiwa una maswali yoyote kuhusiana na habari hii tafadhali piga simu shuleni ili upange muda wa kujadiliana.

Mwaminifu wako

Mwalimu Mkuu (Principal)

**Huduma ya Mkalimani wa Simu**

Ikiwa ungetaka maelezo zaidi na unahitaji mkalimani kukusaidia na swali lako, tafadhali piga simu kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa 131 450 na omba kwa mkalimani katika lugha yako. Umwambie mwendeshaji wa simu namba ile ya simu unayotaka kupiga simu na mwendeshaji wa simu atapata mkalimani kwenye laini kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii..